

SABABU NYINGINE MUHIMU SANA ILIYOMFANYA YA
YESU KRISTO AKAE NA WANAFUNZI WAKE SIKU 40
BAADA YA KUFUFUKA NI ILI AWATHIBISHIE WALE WOTE
WATAKAOJITOA NA KUMTUMIKIA KUWA YEYE
ATASHUGHULIKIA MAHITAJI YAO YA MWILINI PIA.

MAANDIKO: Yoh. 21: 1 – 14.

- Huko nyuma Yesu alishakutana na maswali magumu na akayajibu. **Math. 19: 27 – 29**, lakini hata Nabii Malaki alikutana na watu waliokuwa na maswali magumu na kisha wakaacha kabisa wokovu. **Malaki 3: 13 – 18.**
- Ni dhahiri kabisa kwamba Yesu alipoteswa na kisha kufa kwa aibu pale msalabani, wanafunzi wake walikata tamaa, na wakaona wamepoteza muda wao wa kutembea na Yesu **miaka 3^{1/2}** yote bure na anawaacha mikono mitupu!!! **Waliona wazi kwamba kumtumikia Mungu ndiyo chanzo cha wao kufilisika; kubakia mtu duni na asiye na mwelekeo tofauti na wala rushwa na wafanya magendo na mafisadi ambao maisha yao yanawiri kila kukicha!!**
- **Kwa hiyo Yesu anajidhihirisha kwao wakati wameamua kurejea kwenye kazi zao bila kupata kitu usiku kucha ili awathibitishie kwamba kumtumikia yeye ndiyo chanzo cha Baraka zote za mtu ziwe za rohoni au za mwilini.**
- Yesu anaonyesha kujali hata kifungua kinywa chao (breakfast) na kufanya mambo ya kuwashangaza Mitume hawa kwa lengo la kutaka sasa wawe na mtazamo wa mambo ya Mungu kiroho zaidi wakati wote watakapokuwa wakimtumikia; alikuwa anawajengea tabia ya kupokea maelekezo kutoka kwa Bwana katika kazi zao kama wanataka kupata mafanikio; na wajue kwamba nje ya

Yesu mengi watakayokimbizana nayo kuyafanya yataishia katika utupu na kushindwa na kupoteza nguvu zao bure.

Note: Kumbadilisha mtu kutoka tabia za asili alizozaliwa nazo ni jambo gumu sana; hadi Roho Mtakatifu amkalie ndipo anapowezekana. Yoh. 3:3

- Ndiyo sababu Yesu alipokutana na Wanafunzi wake tu kasoro Tomaso kwa mara ya kwanza kule Galilaya wakiwa wamefunga milango ya nyumba kwa hofu ya kuwaogopa Wayahudi, aliwaambia mara mbili – amani iwe kwenu na **AKAWAVUVIA** na kuwaambia **POKEENI ROHO MTAKATIFU . Yoh. 20: 17 – 23.**
- **Neno kuvuvia** ni sawa na neno lilivyotumika wakati wa kuubwa kwa Adamu – **Mwanz. 2:7 (Emphusao)**. Kama ambavyo Mungu alipulizia pumzi ndani ya Adamu na Adamu akawa nafsi hai kimwili, Yesu sasa anawavuvia ili wawe hai Kiroho (wawe viumbe vipya, wawe na mtazamo mpya wa mambo tofauti na walivyokuwa wanayafahamu. **2Kor. 5:17**
- Ndiyo maana ya kuokoka; mtu anapookoka, Yesu anaihuisha roho yake iliyokuwa imekufa na mtu anafanyika nafsi hai tena ili aweze kuyafahamu na kisha kuyatenda mapenzi ya Mungu. **1Kor. 15: 45, 2Kor. 3: 12 - 12 Yoh. 6: 63.**
- Ni wakati huu alipokutana nao baada ya kufufuka kwake, Yesu Kristo, sasa anawavuvia ili wampokea Roho Mtakatifu yaani wazaliwe upya Kiroho, na hii ni tofauti

kabisa na kubatizwa na Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste. **Mdo. 2: 1 – 4.**

- Kabla ya Yesu Kristo kuwatokea wanafunzi wake baada yakufufuka; walikuwa ni wanafunzi waliomfuata Yesu kulingana na namna ya Agano la Kale; na wao wasingeweza kumfuata Yesu kulingana na Agano Jipya maana Agano Jipya limepatikana kwa njia ya kufa na kisha kufufuka kwa Bwana Yesu. **Efeso 2:11- 20, Ebr. 9: 11 – 16, Luk. 22: 20 (Math. 26: 27 – 28)**
- Mitume hawa 11 wakawa ndiyo wazaliwa wa kwanza kiroho baada ya Yesu kufufuka na kuwavuvia ili wampokee Roho Mtakatifu; kuanzia siku hii ndipo Kanisa la kwanza la Agano Jipya likazaliwa; ambalo litakuwa na mtazamo mpya tofauti na Kanisa la Agano la Kale ambalo lilikuwa na mtazamo wake kama tulivyoona katika **2Kor. 3: 12 – 18**

Note: Kumwagwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste **Mdo. 2:4** ni tukio lililo watokea wanafunzi wa Yesu baada ya wao kufanywa wapya (kuongoka/kuokoka) baada ya kuvuviwa na kufanywa upya kiroho na Roho Mtakatifu.

- Na huu ndiyo utaratibu kwa waumini wote wa Yesu Kristo duniani tangu wakati huo; Roho Mtakatifu anaingia ndani yetu pale tunapompokea Yesu Kristo ili awe Bwana na mwokozi wetu ili tuzaliwe upya Kiroho (tuwe viumbe vipya) halafu hatua ya pili ni kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa ajili ya kupokea nguvu ili tuweze kuwa

mashahidi halisi wa kweli ya Injili ya Yesu Kristo.
Mdo. 1:5, 8, 2:4.

- Baada ya kufanyika viumbe vipya kiroho na baadae kubatizwa (kujazwa) na Roho Mtakatifu; wanafunzi wote wa Yesu walibadilika kabisa, hakuna aliyeona kwamba kumtumikia Mungu kunaleta hasara, hawakuogopa tena wala kuionea haya injili ya Bwana Yesu Kristo; bali waliona fahari endapo watapata mateso kwa sababu ya Yesu!!! **Mdo. 5:40-42, (Mt. 5: 10-12) 1Pet. 4: 12 – 19.**
SISI TUKOJE LEO!!! TUMEVUVIWA!!! TUMEBATIZWA NA ROHO MTAKATIFU!!!! TU VIUMBE VIPYA!!!

NA

Askofu Dr. L. Mwizarubi

May 2021